

Moderato

# NITAHUKUMIWA MWENYEWWE

Na. Joseph Rimisho  
2011  
Arusha

## Shairi

1. Ni me si ma - ma gha fla ni ka ji u li za!  
Ni ma mbo ga - ni ni me fa nya du ni a ni?

Ka bla ha i ja fi ka - si ku ya nu ku mu,  
Ndi po ni ta we ka ma mbo ya ngu yo te wa zi,

U ta fi ka wa ka ti wa ku hu ku mi wa,  
Ni ta to a he sa bu ya ma te ndo ya ngu,

## KIITIKIO

Ni ta hu ku mi wa kwa ma te ndo ya - ngu mi mi  
mi mi

Ni ta hu ku mi - wa mwe nye - we!

2. Kama matendo yangu yalikuwa haba,  
Sikuyatenda yanipasayo imani,  
Mbele ya hukumu sina neno la kujibu,  
Wala hakuna atakayeweka dhamana,  
Jambo moja la heri bado niko hai,  
Nizishike amri za Mwenyezi Mungu,  
((Nitahukumiwa(mimi) kwa matendo yangu  
(mimi) nitahukumiwa mwenyewe))x2

3. Nikitazama pande zote za dunia,  
Napata hofu nionapo vishawishi,  
Nikiyakumbuka maagizo yake Mungu,  
Nazo ahadi za kumkataa shetani,  
Nitashika kiapo wala sitaacha,  
Nitavipiga vita vilivyo vizuri,  
Nitahukumiwa.....

4. Tazama zipo siku mbaya zinakuja,  
Ambapo utaita BWANA uko wapi?  
Nuru ya- jua itakapozi-mika,  
Mwezi nazo nyota hazitamulika tena!  
Mwisho umeshafika unangoja nini?  
Uhodari na nguvu vimeshatoweka!  
Nitahukumiwa.....

5. Neno imara ni kukesha kwa kuomba,  
Sikutimiza muda wangu umekwisha,  
Sitasu-biri yanifike ma-baya,  
Nitafanya kazi ya imani ma-pema  
Nijiweke tayari arudipo Bwana,  
Anikute ni msafi sina dhambi tena,  
Nitahukumu.....

6. Kama ni vita mimi nimeshapigana,  
Safari yangu ikifika msilie,  
Kaburini nimekwenda wala sitarudi,  
Zitengenezeni njia zenu ma-pema,  
Waiteni na ndugu waje kwake Yesu,  
Wayatubu makosa wasitende dhambi,  
Nitahukumiwa.....

7. Sikia ndugu nisemapo mambo haya,  
Hakika leo tupo hatujui kesho,  
Tukeshe kuomba na kutubu dhambi zetu,  
Mungu ana fadhili na huruma ya kweli,  
Tukifika mbinguni heri yetu sisi,  
Tutaishi milele tukimsifu Mungu,  
Nitahukumiwa.....

KILA NAFSI ITAONJA MAUTI  
JIWEKE TAYARI MAPEMA

Umenakiliwa upya leo tarehe  
15.09.2014.....1320hrs  
Monduli-Arusha  
Mimi Joseph Rimisho nimeandika

TUNZA MUZIKI WA KANISA  
Sunday Morning Organist